

**Ninapaswa kuwasiliana na nani ikiwa nina
masuala kuhusu kesi yangu ambayo hayawezi
kusuluhishwa na mto huduma za jamii wa FVS?**

Ikiwa una suala au malalamiko kuhusu jinsi kesi yako inavyoshughulikiwa, wasiliana na msimamizi wa mto huduma wako wa jamii wa FVS. Ikiwa bado masuala yako hayajashughulikiwa, unaweza kuwasiliana na Msimamizi wa Eneo.

Pia unaweza kupiga simu kwenye Ofisi ya Mahusiano ya Washiriki kuitia 800-723-4831 au 360-902-8060 upate usaidizi wakati wowote.

Department of Children, Youth and, Families (Ofisi ya Mchunguzi wa Umma wa Watoto na Familia) ya Jimbo la Washington hupokea masuala na malalamiko kuhusu shughuli za Idara ya Watoto, Vijana na Familia na ina mamlaka ya kuchunguza madai. Unaweza kuwasiliana nao kuitia 800-571-7321.

**Ili upate maelezo zaidi,
tembelea:**

<https://dcyf.wa.gov/services/child-welfare-system/cps>



Maelezo ya Mhudumu wa Jamii:

Jina: _____

Simu: _____

Barua pepe: _____

Maelezo ya Msimamizi wa Mhudumu wa Jamii:

Jina: _____

Simu: _____

Barua pepe: _____



Tafuta ofisi ya DCYF iliyo karibu nawe:


Changanua Msimbo wa QR, au uende kwenye:
<https://apps-ca-ext.dcyf.wa.gov/CAOfficesPub/offices/general/OfficePick.asp>

Ikiwa ungependa nakala za chapisho hili bila malipo katika miundo au lugha imbadala, tafadali wasiliana na DCYF Mahusiano ya Washiriki kwa 1-800-723-4831 au barua pepe kuitia communications@dcyf.wa.gov.

DCYF PUBLICATION CWP_0035 | DSHS 22-1751_SI (03-2025) Swahili

Family Voluntary Services (Huduma za Kujitolea za Familia)

Kuimarisha Familia Kupitia Ushirikiano wa Kutoa Huduma na Rasilimali Saidizi



Washington State Department of
CHILDREN, YOUTH & FAMILIES

Family Voluntary Services (Huduma za Kujitolea za Familia, FVS) ni nini?

FVS ni mpango ambao unawawezesha wazazi/walezi wa kisheria kushiriki katika huduma za kutimiza mahitaji ya usalama, afya na ustawi wa (mtoto) watoto wao.

Lengo la FVS ni kuzisaidia familia kushiriki katika huduma zinazowezesha kukidhi mahitaji ya familia huku tukiziimarisha na kuziweka familia pamoja.

Wahudumu wa jamii hushirikiana na familia ili kukamilisha tathmini ya uwezo, mahitaji, na usalama wa watoto. Familia zinaweza kuchagua kuacha kushirikiana na Department of Children, Youth and, Families, DCYF (Idara ya Watoto, Vijana na Familia) wakati wowote. Ikiwa familia itachagua kusitosha huduma za FVS, wahudumu wa jamii wanatakiwa kutathmini kiwango cha usalama na hatari kabla ya kufunga kesi. Ikiwa kuna hitaji ambalo halijatimizwa linalohusiana na usalama wa watoto, DCYF inaweza kuiomba mahakama kuingilia kat kwa kuwasilisha ombi la utegemezei.

Mpango wa FVS hufanya kazi vipi?

FVS inaweza kutolewa kufuatia kesi ya CPS wakati huduma na nyenzo zinaweza kuzisaidia familia ili kuhakikisha usalama wa watoto na uthabiti wa familia.

Familia pia zinaweza kuomba huduma za FVS zinapohitajika kwa kupiga simu kwa DCYF.



MATARAJIO

Mambo ya kutarajia kutoka kwa mto huduma wako wa jamii wa FVS

- Ataihudumia familia yako kwa heshima.
- Kushirikiana na wewe na kufanya mpango wa kudumisha usalama wa watoto wako na kuhakikisha watoto wako wanakidhiwa mahitaji yao ya kimsingi.
- Atakupa mahususi wewe na kwa familia yako, kama vile elimu ya uzazi, ushauri nasaha; au matibabu. Tembelea tovuti ya DCYF uone orodha ya kina zaidi ya huduma na rasilimali.
- Atakutana na familia yako na pia kukutana na watoto kwa faragha nyumbani kwako angalau mara moja hadi mbili kwa mwezi.
- Atawasiliana na watoa huduma, washirika wa jamii, familia na marafiki (kwa ruhusa yako) ili kupata mtazamo wa nje kuhusu maendeleo yako na ya familia yako.
- Atazungumza nawe kuhusu usalama wa kibinasi na wa watoto wachanga/wazaliwa.
- Ikiwa mtoto wako anashukiwa kunyanyaswa kingono kibiashara, atakusaidia kufanya tathmini na kukupa huduma.
- Atakuhimiza kushirikiana na mshirika mwenza au kuhudhuria kikundi cha usaidizi kila inapowezekana.

Mambo ambayo mto huduma wako wa jamii wa FVS anatarajia kutoka kwako

- Kushiriki katika mchakato wa tathmini na kusaidia kkuza mpango wa kuimarisha ustawi wa familia yako na uthabiti wa muda mrefu.
- Kufuata mpango wa usalama (iwapo upo).
- Kushiriki katika huduma za kuimarisha ustawi wa familia yako na uthabiti wa muda mrefu.
- Kuruhusu mto huduma za jamii wa FVS kukutana na watoto wako kwa faragha.
- Kukutana na mto huduma za jamii wa FVS mara kwa mara.
- Kuendelea kufahamisha mto huduma za jamii wa FVS kuhusu mabadiliko yoyote katika hali yako.
- Kutia saini ya kutolewa kwa maelezo yako na ya watoto wako.
- Kushiriki maelezo kuhusu uwezo, mahitaji na hali za familia yako.